CHAMBUZI ZA MWALIMU WA LUGHA

Utangulizi

Shaekha Barrack Mamba ni mmojawapo wa watunzi wapevu wa karne hii.Mwenyezi Mungu alimpokeza upawa naye akaupokea kwa mikono miwili. Ni kielelezo kwa vijana wanaopenda mashairi kuwa mashairi si ya wakale tu kwani yamepokezwa kwa mtu wa hirimu lao pia.malengo yake makuu ni kuondoa magezo kuwa Kiswahili ni lugha finyu na amewajibika katika kushughulikia vipengee ambavyo wakale wake hawakuvishghulikia vyema au waliacha mapengo tuyajaze sisi(wanamapinduzi).Hii ndiyo hatua yake ya kwanza kuhakikisha kuwa Kiswahili hakibezwi.Akramu Muadhamu aibariki kazi ya mikono yake.

SHAKHA MSIKICHO

Barrack Shakha alizaliwa mwaka wa 1993 mnamo mwezi wa kumi tarehe kumi na mbili katika mji wa Bungoma.alizaliwa kama mwana wa tatu wa Bi. na Bw. Richard Oduor.alienda katika shule ya msingi ya khaoya na huko ndiko alikopata ari na mwako wa kutunga mashairi. Kipawa alikipata, akakitunza.
leo hii Shakha Wandera yuko katika kidato cha nne na ameweza kutunga mashuara zaidi ya mia moja ya Kiswahili na zaidi ya mia moja ya kiingereza. Alikipata kipawa hiki baada ya kupenda kusoma mashairi na akayaenzi.alikuzwa na familia ya Jamala lakini hilo halikuwa sababu ya kufisha talanta yake. Ama kweli muungwana akivuliwa nguo huchutama. Jambo lililomuudhi Shakha ni kuwa alipojaribu kuungana na wakenya wenzake ili waikuze talanta walinyamaa.
Swali ni je aliwezaje kupata ufariji? *Ama kweli Mungu si Athumani. Alipatana na mmarekani Courtney Harms ambaye alimfanikisha na kumwinua nyota huyu.Shabash!*

ISTILAHI ZA KISHAIRI NA FASIHI

Istilahi za kishairi

ushairi*-sanaa ya utunzi wa mashairi, tenzi, ngojera n.k*
Shairi(1)*-mtungo wa kisanaa wenye mpangilio wa kipekee wa lugha ya mkato katika semi, maandishi au wia unaoelezea tukio au matukio Fulani katika jamii,au hoja fulani, au hisia fulani, au umbile fulani na ambao hufuata utaratibu wa urari na muwala maalum kwa kuheshimu na kuzingatia kunga, tamaduni na kanuni za utunzi wa mashairi uanaohusika.*
Shairi(2)*-rekodi zilizosukwa za mambo yaliyotokea(kadhia)ambayo huwa na urari wa mizani na vina na ambao hufwata mtiririko na arudhi za kishairi.*
Shairi[3]*-pia huweza kuelezwa kama habari zilizofupishwa za mambo yanayowazingira wanadamu.*
Wia-*wimbo au utenzi ambao hauna vina na mizani*
Wimbo- *maneno au maandishi yanayotamkwa kwa sauti ya kimziki. Huambatana na malenba katika kazi yake. Huundwa kutokana na mahadhi.*
Mahadhi- *upandishaji na ushukaji wa sauti katika uimbaji.*
Utunzi- *sanaa inayohusika na ubunifu wa kiwango cha juu.*

CHAMBUZI ZA MWALIMU WA LUGHA

Utungo(tungo)-*kazi ya sanaa inayotumia lugha k.v. shairi, wimbo, tenzi,semi, n.k.*
Semi*-fungu la maneno linalotumiwa na jamii fulani ya watu kwa namna maalum kutoa maadili.*
Sanaa-*ufundi wa kuwasilisha hisia na mawazona hoja za kibinadamu kwa maandishi, michoro na uchongaji*
Lugha-*mpangilio wa sauti na maneno unaoleta ambayo hutumiwa na watu wa jamii au nchi fulani kwa minajili ya kuwasiliana*
Sauti-*msuguano wa ala za kinywa cha kiiumbe ili kutoa mlio*
Urari-*usawa ,ulinganifu na upasao wa vipengele vya kisanaa k.v. mizani*
Hoja- *swala lolote ambalo msanii anweza kutumia kujenga mada yake*
Tukio(kadhia)*-jambo lolote lilofanyika au kutokea katika historia.*
Ustadhi*-lina maana mwalimu na mizizi yake iko uarabuni.*
Bahari- *aina za tungo za kishairi kama utenzi, tarbia, mandhuma, msemele, n.k.*
Diwani-*kitabu cha ushairi m.f. diwani ya Msikicho,*
Muktadha- *jambo au habari inayozungumziwa*
Jazanda-*mfano, taswira au picha ya kufananisha kitu chochote na binadamu na kukipa sifa, tabia au nafsi ya kibinadamu*
Gungu*-shairi lenye mishororo mirefu na mizani mingi[zaidi ya mizani 12]na kila mshororo una kina kimoja tu cha mwisho.*
Guni*-shairi lililolemaana lililotungwa bila kufwata arudhi za ushairi-haufwati kanuni.*
Maudhui-*mambo muhimu yanayozungumziwa katika shairi k.v mapenzi,usalit,uhayawanin.k*
Dhamira/maudhui-- *munikuunda lengo kuu au jambo linalomsukuma mwandishi kazi yafasihi.mf. Kuonya vijana katika jamii kutokananana mapenzi ya uongo*
Muwala-mtiririko wa mawazo *kutoka ubeti hadi ubeti.hili hutummiwa kupima upevu wa mshairi.pia huitwa mtiririko.*
Wahusika*-viumbe wanaotumiwa kuendeleza kazi ya fasihu.*
Lugha ya mshairi- *lugha ya ya mkato hutumiwa.ni lugha ya kipekee.*
Beti*/ubeti-kifungu kimoja cha ushairiaumkusanyiko wa mishororo unaodondoa hoja kishairi.*
Mshorororo*-mstari upatikanao katika ubeti wa ushairi.*
Kibwagizo*-mkarara au mstari wa mwisho unaorudiwarudiwa katika kila ubeti.*
Mizani*-idadi yasilabi au mapigo katika mshororo wa ushairi.*
Vina*-sauti zinazofanana katikati na mwisho wa mshororo wa shairi.*
Ukwapi-*kipande cha kwanza cha mshororo.*
Utao*-kipande au sehemu ya pili ya mshororo.*
Mwandamizi-*kipande cha tatu cha mshororo.*
Mwanzo*-mshororo wa kwanza wa ubeti.*
Mloto*-mshororo wa pili katika ubeati.*
Mleo-*mshororo watatu katika kinyingina ubeti wa shairi.*
Kinying'ina/kipokeo /Kibwagizo/ kitikio *-mshororo unaorudiwarudiwakatika kila mhororo wa ubeti.*
lugha nathari- *lugha ya riwaya ambayo ni maelezo tu wala si ya kishairi.*
Utoshelezi*-hali ya ujumbe katika ubeti kujisimamia bila kuegemea ubeti mwingine.*
Urari*-hali ya kulandana au kufanana kwa vina na mizani*
Arudhi*-sheria au kanuni zinazofwatwa katika utunzi wa mashairi.*

CHAMBUZI ZA MWALIMU WA LUGHA

***Wanamapinduzi**-watunzi wa siku hizi ambao aghalabu hupenda utunzi wa mauve.*
***Mgao**-kipande cha mshororo*
***Tanuwini**-mbinu ya kuweka sauti ya 'n' mwishoni mwa neno isipokuwa kwa kuleta urari wa vina na mizani kwa minajili ya kuremba lugha mf.* **Teleka** *kuwa* **telekan**.

Uhuru Wa Shakha
***1.Uhuru wa mshairi**- uhuru ambao mshairi anao kutoka kwa sintaksia.*
***2.Inkisari**-mbinu ya kupunguza idadi yaya silabi katika neon.*
***3.Mazida/mazda**-mbinu ya kurefusha idadi ya silabikatika neno.mf Yesu kuwa Yesusi.*
***4.Tabdila**- mbinu ya kubadili herufi katika neno.mf harara kuwa harari.*
***5.Matumizi ya lahaja-**tofauti kati ya matamshi ,maumbo na matumizi ya lugha yenye asili moja.mshiri /shakha maneno katika lahaja tofauti na ile ya kiunguja iliyosanifishwa.*
Mf katika lahaja ya kiunguja- **makao** *kuwa* **machao**
*Lahaja ya chifundifundi-***sasa** *kuwa* **tsatsa.**
*Lahaja ya kibajuni-***pete** *kuwa* **peche**
*Lahaja ya kimvita-***njia** *kuwa* **ndia.**
***6.Utohozi**-mbinu ya kuchukua neno au maneno kutoka lughanyingine na kupachika kwa lugha ya Kiswahili.*
***7.Tanakali za lafudhi**-mshairi ana uhuru wa kutunga bila kuzingatia athari za lugha ya mama mf kama ni mluhya basi anaweza kusema* **ukali** *badala ya* **ugali.**
***8.Matumizi ya Kiswahili cha zamani**-mfano* **macho** *kuwa* **maozi**,**goti** *kuwa* **moo.**
***9.Kuboronga sarufi/kufinyanga sintaksia**-kubadili mpangilio wa fungu la maneno mfano shaekha ametunga mashairi kuwa mashairi shaekha ametunga.*
10. ***Mbinu ya mubadala**-kutumia neon au maneno mengine yenye maana sawa (visawe) nay ale ya kawaida ili kupata urari wa vina na mizani.mfano=*

Kataa *kuwa* **kana**
Finya *kuwa* **bana**
Ongea *kuwa* **nena**

***11.Ubadilishaji wa maneno ya lugha nyingine kuleta kwa Kiswahili ukizingatia muundo wa neno hilo.**mf*

Net-work *jina la kingereza*
Net *ni wavu kwa Kiswahili*
Work *ni kazi kwa Kiswahili*

Hivyo basi **network** *kuitwa* **wavukazi** *na mshairi.*

Mobilephone *jina la kingereza*
Mobile *ni tamba au inayotanga*
Phone *ni simu.*

Hivyo basi **mobilephone** *kuitwa* **simutamba** *na mshairi.*
*12.****mtumizi ya ritifaa au vin'gon'go***
Mshairi ana uhuru wa kufupisha neno akitumia ritifaa au vin'gon'go.mfano

Nitaenda *kuwa* **n'taenda**
Asiyenijua *kuwa* **asiyen'jua**

*13.****matumizi ya tanuwini***

CHAMBUZI ZA MWALIMU WA LUGHA

Mshairi ana uhuru wa kuongezea sauti ya 'n' ili kuyaremba mashairi yake kando na kupata urari wa vina na mizani.mfano
Juma alienda soko *kuwa* **Juma alienda sokon**

VISAWE VYA ARUDHI

kanuni za ushairi
Kaida za ushairi
Ada za ushairi
Kunga za ushairi
Itikadi za ushairi

LAHAJA ZA KISWAHILI
1.kibarawa
2.kisiu
3.kishela
4.kiamu
5.kipemba
6.kihadimu
7.kipate
8.kingwana
9.kingazija
10.kimwani
11.kimvita
12.Kimtang'ata
13kimrima
14.kimgao
15.kikae
16.kijomvu
17.kihadimu/kiadimu
18.kibajuni
19.kisiu
20.kiunguja
21.kivumba
22.chimiini
23.kimashomvi
24.kingunya
25.kimakunduchi
26.kitumbatu
27.kingozi
28.kitanga
29.chifundifundi
30.kibajuhi/kitikisiu
Aina za mashairi
Masivina-*shairi lililo na urari wa mizani wala sio wa vina.*

CHAMBUZI ZA MWALIMU WA LUGHA

***Mauve**-shairi lisilofwata arudhi za ushairi elakini lina mtiririko na utoshelezi.*
***Pindu**-katika shairi hili kipande cha mwisho cha mshororo hutumiwa kuanzisha kipande cha kwanza cha mshororo unaofwata.*
***Ukawafi**-shairi amalo limegawika katika vipande vitatu.*
***Mathnawi**-shairi ambalo limegawika katika vipande au migao miwili.*
**__ukangou/bantudi__-shairi ambalo limegawika katika vipande viwili.*
**__ukiyani__- shairi ambalo mbinu ya kinaya imetawala beti zake.*
***Mandhuma**-shairi ambalo swali hutolewa katika ukwapi na jibu kutolewa katika utao.*
***Ukaraguni/mkaraghuni**-urari wa vina na mizani huwepo katika ubeti japo havilandani katika shairi zima.*
***Msuko**-shairi ambalo kibwagizo chake kimesukwa.*
***Ukara-**iwapo vina vya ndani vinalandana na vya nje havilandani auvya nje vinalandana na vya ndani havilandani basi shairi hili ni ukara.*
***Mtiriko**-vina vya ndani na vya nje hulandana katika shairi zima.*
***Kikwambaa**-shairi linaloanza kwa neno moja katika kila mshororo wa betize.*
Sabilia/mkarara-shairi ambalo kiishio hurudiwarudiwa katika kila ubeti.
***Sakarani**-shairi ambalo limechanganya bahari zaidi ya moja k.v sabilia na sakarani.*
***Tumbuizo**-aghalabu huwa na migao mitatu kwani mshairi huwa na upevu wa kupanga maneno vizuri ili yalete mvuto kwa msomaji.*
Malumbano-wahusika huchunguzwa katika shairi,ujumbe pia na huwa na majibizano ya kishairi.
***Kikai**-ukwapi huwa na mizani minane ilhali utapo una mizani mine.*
***Ngonjera**-shairi lenye majibizano na aghalabu huandamana na viashiria.*
***Ukumi**-bahari yenye upevu wa juu sana,huwa na mishororo kumi katika kila ubeti.*
****kumbada**-kwa malenga waliopevuka zaidi(shakha).huwa na mishororo zaidi ya kumi katika kila ubeti.*
***Tathmina**-shairi lenye mshororo mmoja katika kila ubeti.*
***Tathnia**-shairi lenye mishororo miwili katika kila ubeti.*
***Tarbia**-shairi lenye mishororo mine katika kila ubeti*
***Takhmisa**-shairi lenye mishororo mitano katika kila ubeti.*
***Tashlita/tasdisa**-shairi lenye mishororo sita katika kila ubeti.*
****mbumbuki**-shairi ambalo maudhui ya kijinga yamelitawala.*
****timbeba**-shairi ambalo mshororo wa kwanza wa kila ubeti hubebwa na kupachikwa mwishoni mwa ubeti hivyo basi kufanywa ukingo japo haurudiwirudiwi.*
****badrudi**-shairi ambalo kwalo mshororo wa kiwango fulani huwa na urari wa vina na mizani ,iwapo ni mshororo wa kwanza basi huwa hivyo.*
****Makhbaha**-shairi amalo limesheheniwa na mbinu ya tashbihi.*
***Mapingiti**-tungo za kishairi zilizolemaa kabisa.lina kasoro katika maudhui,urari,muwala na dhamira yake.*
Hamziya/*umhaji**-mbinu ya tathnia imeshamiri japo mizani yake huzidi 24 na aghalabu huwa na kina cha **‘ma’
***Kasida/*hadmini**-maudhui ya kidini yameshamiri katika shairi hili.*
***Naudi/*unane/*tahnini**-huwa na mishororo minane.*
***Telemania/utisa/*tasnini**-huwa na mishororo tisa.*
***Tasbia/usaba**-huwa na mishororo saba katika kila ubeti japo ni adimu.*

CHAMBUZI ZA MWALIMU WA LUGHA

Kumbukizi/makmbumbu*-huhusishwa na kadhia yoyote kubwa .hutujuza au kutuletea kumbukumbu za kadhia kama vita vya ukabila vyakenya mwaka 2007 katika shairi la Arshi katika diwani ya Msikicho.*
Kisarambe*-shairi linalozungumzia mambo ya uungu.*
Kikai*-hujitokeza kwa namna nyingi.mizani 12.yaweza kuwa 8.4,4.8,6.6 n.k*
Kiambo*-huzungumzia mazingira Fulani mf msitu wa kakamega,bahari ya hindi n.k*
Taabili*-shari lililotungwa kwa madhumuni ya kimsifu aliyeaga dunia.*

<u>Istilahi za fasihi</u>

Mgogoro*-ni hali ya kutoelewana na kutoafikiana baina ya pande mbili kama ni wahusika basi baina ya wahusika wawili au zaidi.*
*****mikwala****-pingamizi au vizingitikatika kufanyika kwa jambo fulani haswa linalowakumba wahusika wa kifasihik.vvizingiti dhidi ya ukombozi wa wanawake.*
Tenzi(utenzi)*-utungo mrefu wa kishairi unaoelezea hitoria au kadhia fulani na ambao hauna vina vya kati katika mistari yake japo una vina vya nje*
Tendi(utendi)*-utungo mrefu wa kishairi ambao unamsifu na kumpemba shujaa wa kipekee. mf shakha BaR katika diwani ya Msikicho.*
Majazi*-mhusika hupewa jina kutokana na matendo au mwenendo wake.*
Taswira*-jazanda au mbinu ya kuchora picha akilini mwa msomaji.*
Chuku*-mbinu ya kuongeza chumvi ili kuvutia msomaji.*
Tasfida/usafidi/tauria*-mbinu ya kutumia lugha isiyoleta ukali wa maneno.*
Tanakali za lafudhi*-kuonesha athari za lugha ya mama.*
Tabaini*-mawazo yanayokinzana ili kuleta msistizo mf. Lila na fila havitangamani.*
Semi*-hutumiwa katika ushairi kuongeza ladha na kuleta mvuto kwa msomaji.fungu la maneno lenye maana fiche.mf*
Ana kichwa kizito-***ana kiburi***
Mkono birika-***ana choyo***
Mubalagha*-maswali yasiyohitaji majibu hutumiwa na mshairi ili kuwasilisha ujumbe wake.*
Utohozi*-uwasilishaji wa neno la lugha nyingine katika Kiswahili(kimatamshi na kimaandishi)*
Mf **computer** *kuwa* **kompyuta**
Mjalizo*-matumizi ya sentensi zisizo na viunganishi vyovyote.*
Alilima,akachoka,akaoga,akalala
Vilivyaywa,vikatupwa,vikaugua,vikafa
Jazanda*-lugha ya kimafumbo.hueleza jambo ukitumia viyu vya kawaida japo vilivyobeba maana fiche*
Tadmini*-lugha zaidi ya moja hutumiwa katika kuwasilisha ujumbe kimaandishi na kishairi.*
Takriri/msisitizo bayana*-neno au fungu la maneno hurudiwarudiwa ili kusisitiza ujumbe.*
Mf
Muadhamu orabada,mwangata wa mafakiri
Muadhamu orabada,mrithi wa ushairi
Muadhamu orabada,malenga wa lugha nzuri
Muadhamu orabada,kijana mwenye nadhiri

CHAMBUZI ZA MWALIMU WA LUGHA

Tashibihi/mshabaha*-kufananisha kitu na kingine kwa matumizi ya 'kama', 'mfano wa' ,'mithili ya' n.k*
Mf orabada ni jasiri kama samba.
Tanakuzi-*matumizi ya maneno yanayokinzana.mf adui mpende.*
Methali*-fungu la maneno lenye maana finye na ya busara.mshairi ana uhuru wa kukwepa kutumia methali halisi kama ilivyo.mf*
Asiyesikia la **mkuu** *huvunjika* **guu** *kuwa asiyesikia la* **mzazi** *huona* **makuu.**
Tashhisi /uhaishaji-*kukipa kidude chochote sifa na tabia za kibanadamu.mf*
Jiwe *lisilo* **adabu,***lilimuadhibu kaka.*